



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MJI NANYAMBA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

Simu
Barua pepe: td@nanyambatc.go.tz

S.L.P 1490,
NANYAMBA-MTWARA

Kumb. Na I.95/338/03/54

Tarehe 28/07/2020

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Mji Nanyamba imepata kibali cha Ajira mbadala chenye Kumb. Na.FA.170/362/01/A/27 cha Tarehe 02 Julai, 2020 kwa ajili ya kuajiri watendaji wa Vijiji watatu (3).

Hivyo, Mkurugenzi wa Mji Nanyamba anawatangazia watanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Mji Nanyamba, kuomba nafasi za kazi za Mtendaji wa Kijiji kuanzia leo Tarehe 28 Julai, 2020.

2.0 MTENDAJI WA KIJIKI/MTAA DARAJA LA III - TGS B (Nafasi 3)

2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya cheti (Astashahada) katika moja ya Fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

2.2 MSHAHARA

Ngazi ya Mshahara ni TGS B1.

2.3 KAZI/ MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI


- i. Afisa masuuli na Mtendaji wa Serikali za kijiji.
- ii. Kusimamia ulinzi wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa amani na usimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- iii. Kujibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia sera na taratibu
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji na kazi katika eneo lake na kuhamasisha uchumi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi mkuu wa Idara na Vitengo vya kitaaluma katika Kijiji.
- viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka za Kijiji.
- ix. Kupokea , kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi

- x. Kusimamia ukusanyaji wa mapato katika Kijiji.
- xi. Kuandaa na kutunza Rejesta ya wakazi wote wa Kijiji.
- xii. Pamoja na kazi zingine utakazopangiwa na Mwajiri wako.

2.4 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu.
- iv. Maombi yote yaambatane na picha 2 (passport size), nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoелеkezwa hapo juu.
- v. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NACTE na NECTA).
- vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Mamlaka husika.
- viii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 10 Agosti, 2020 saa 9.30 alasiri.**
- ix. **Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.**
- x. Maombi yote yatumwe kwenye anuani ifuatayo;

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji Nanyamba,
S.L.P 1490,
NANYAMBA-MTWARA.



Thomas E. Mwaifafu
MKURUGENZI WA MJI

NANYAMBA
MKURUGENZI WA MJI
HALMASHAURI YA MJI
NANYAMBA